**MODULE 1**
**UTANGULIZI WA KOMPYUTA**

Top of Form

---

Bottom of Form

**TARAKILISHI** AU **KOMPYUTA**

ni mashine au chombo cha kielektroniki chenye uwezo wa kupokea na kukusanya taarifa (data), na halafu kuzishughulikia kulingana na kanuni za programu ya kompyuta inayopewa. Inafuata hatua za mantiki katika kazi hii. Hapo hutoa matokeo ya kazi hiyo na namna ilivyoendeshwa, pamoja na kutoa matokeo ya kitu kilichofanyika, yaani kinachoonekana (Information) kwa haraka. Kimsingi tarakilishi ni kifaa chochote kinachomsaidia binadamu kufanya hesabu. Zipo tarakilishi za aina mbili: za kianalojia (za umakanika) na za kidijiti (za elektroniki). Za kwanza hazitumii umeme, na ndizo ambazo zilianza kabla ya tarakilishi za kidijiti (zinazotumia umeme).

**Tofauti kati ya data na habari (information)**

***Data***

Ni ibara ya taarifa au maelezo, na inaweza kuonekana kwa sura
ya maandishi, michoro, picha, namba, alama, nembo, sauti au lughaya maandishi, au sauti pamoja na picha.

***Habari (Information)***

Ni kazi inayotokana na taarifa au maelezo (Data) baada ya kwisha kupangiliwa na kufanyiwa kazi hadi kutoa matokeo kamili ya kazi hiyo, pamoja na kuleta kitu chenye kufahamika na chenye faida. Ni kazi iliyokwisha kutengenezwa hadi ikawa katika hali ya kueleweka.

**SIFA ZA KOMPYUTA**

**Wepesi**

Kompyuta inafanya kazi kwa wepesi wa hali ya juu kiasi kwamba unaweza kutafuta kitu kwa muda wa sekunde chache tu, kitu ambacho kama utakitafuta kupitia chombo kingine unaweza kuchukua wakati mrefu mpaka kukipata, na pengine usikipate, kwa mfano unaweza kufanya hesabu ngumu kwa muda mchache kuliko kutumia akili yako.

Pia unaweza kutafuta somo lolote kupitia intaneti kwa kutumia muda mfupi kulipata somo hilo kuliko ungetumia marejeo ya vitabu vya kuchapishwa.

**Ubora**

Kompyuta inafanya kazi kwa ubora zaidi bila kuonyesha udhaifu na makosa ya aina yoyote, na kama itabainika ya kwamba kuna makosa yametendeka kwenye kazi yako, kompyuta kabla ya kuendelea kufanya kazi inakuonyesha kwamba upo katika makosa na kukutaka mara moja kurekebisha makosa hayo kwa kukuletea tangazo lenye sehemu kadhaa za kuchagua, ama kuendelea na kazi yako kama ilivyo au kuifanyia marekebisho. Kwa mfano unapotaka kufuta kitu kutoka kwenye kompyuta, kompyuta kabla ya kutekeleza amri hiyo inakuletea tangazo na kukuuliza ya kwamba, ni kweli una uhakika wa kutaka kufuta kitu hicho au umefanya hivyo bila kukusudia?Pia kompyuta imekuandalia kila kitu unachotaka kukifanya ndani yake, kutegemea na malengo yako mwenyewe.Pia kompyuta inazingatiwa ni mwalimu au muelekezaji, kwani inakuelekeza jinsi gani unaweza kufanya kazi yako kwa ukamilifu. Pia ndani ya kompyuta kuna kitu kinachoitwa kisaidizi (help) ambacho kinatumika kwa ajili ya kufanya utafiti wa kitu fulani ili kufahamu matumizi na njia zake.

**Uwezo mkubwa wa kuhifadhi taarifa**

Miongoni mwa mambo muhimu ndani ya kompyuta ni kupatikana sehemu kubwa ya kuhifadhia taarifa kwa amani na bila kuzipoteza.

**Kuhifadhi taarifa**

Kama ilivyotanguliwa kusemwa hapo awali, kuwa kompyuta ni moja ya vyombo vyenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi vitu, na mpaka hivi sasa kuna vifaa ambavyo vinauwezo wa kuifadhi taafira kwa mfano wa vifaa ivo ni diski mweko.

**Kuonyesha matokeo ya vitu (Data na Information)**
Kutokana na maendeleo, elimu ya teknolojia imeweza kurahisisha kazi nyingi ambazo tulikuwa tunazifanya kupitia vyombo mbalimbali. Kila chombo kilikuwa na kazi yake maalumu, tofauti na kompyuta ambapo mtu anaweza kuanzisha au kutengeneza kitu na wakati huohuo anaweza kukionyesha kwa kutumia kompyuta yenyewe, yaani kuonyesha ufanisi na sura nzuri ya kitu kilichofanyika.

## MGAWANYO WA MIFUMO WA KOMPYUTA (CLASSIFICATION OF COMPUTERS SYSTEM)

## 1.MGAWANYO KULINGANA NA UMBO (PHYISCAL SIZE)

### a) Tarakilishi kuu (Super Computer)

Tarakilishi hii inashughulikia kiwango kikubwa kabisa cha hesabu za sayansi.Inahifadhiwa katika chumba chenye mfumo poza maalum ambao unaunganisha uyoyozwaji hewa na kimiminiko poza.
Tarakilishi kuu za miaka ya 1970 zilitumia prosesa (chakataji) chache. Katika miaka ya 1990, zikatokea mashine zitumiazo maelfu ya prosesa. Hadi mwishoni mwa karne ya 20 Tarakilishikuu zitumiazo makumi elfu ya prosesa zikawa ni kawaida. Tarakilishi za karne ya 21 zinaweza kutumia prosesa zaidi ya 100,000 (baadhi zikitumia vizio vyenye kuonesha kwa picha) zikiunganishwa na miungo kasi.Hadi Juni 2013, Tarakilishikuu iitwayo Tianhe-2 ya Uchina, ndiyo yenye kasi kubwa zaidi duniani kwa 33.86 petaFLOPS (*FLoating Point Operations Per Second*).
Mara nyingi mfumo uwezo unaweza kutatua tatizo lenye ukubwa au ugumu ambao hakuna Tarakilishi nyingine inayoweza. Kwa mfano, matumizi magumu sana ya uigaji hali ya hewa.

*Matumizi ya tarakilishikuu*

Hatua za matumizi ya tarakilishikuu zinaweza kuwekwa kwa kifupi katika jedwali lifuatalo:

| Muongo | Matumizi na Tarakilishi husika |
|---|---|
| 1970s | Utabiri wa hali ya hewa, tafita za erodainamiki (Cray-1).[1] |
| 1980s | Changanuzi za Probabilistiki,[2]Ufanyizaji kinga za mnururisho[3](CDC Cyber). |
| 1990s | Mabavu ya uvumbuzi wa maneno ya siri (EFF DES cracker).[4] |
| 2000s | Uigaji majaribio ya nyuklia wa 3D kama mbadala wa utendaji kisheria wa mkataba wa kuzuia ueneaji wa silaha za nyuklia. (ASCI Q).[5] |
| 2010s | Uigaji elimumiendo ya molekuli (Tianhe-1A)[6] |

| Mwaka | Tarakilishikuu | Kasi ya juu (Rmax) | Mahali |
|---|---|---|---|
| 2013 | NUDT Tianhe-2 | 33.86 PFLOPS | Guangzhou, Uchina |
| 2012 | Cray Titan | 17.59 PFLOPS | Oak Ridge, U.S. |
| 2012 | IBM Sequoia | 17.17 PFLOPS | Livermore, U.S. |
| 2011 | FujitsuTarakilishi K | 10.51 PFLOPS | Kobe, Japani |
| 2010 | Tianhe-IA | 2.566 PFLOPS | Tianjin, Uchina |
| 2009 | Cray Jaguar | 1.759 PFLOPS | Oak Ridge, U.S. |
| 2008 | IBMRoadrunner | 1.026 PFLOPS<br>1.105 PFLOPS | Los Alamos, U.S. |

**b)Mainiframu compyuta**

ni aina ya coputer ambayo ina nguvu kiasi yenye gharama ya kawaida kulinganisha na super computer mfano wa matumizi yake hutumiwa na mawakala wa serikali,kampuni kubwa kama benki na hospitali.Tarakilishi kiunzikuu pia inajulikana kama "Chuma Kubwa (Big Iron)" ni ndogo na haina nguvu sana kama Tarakilishikuu katika uwezo wa ukokotoaji. Inahusika na utunzaji wa faili na kumbukumbu kubwa sana.
Tarakilishi iunzikuu zinaweza kuongeza au kufanyia mbadiliko moto uwezo wa mfumo bila kuvuruga utendaji wa mfumo, kwa udhahiri na uchembe wa viwango vya kisasa ambavyo si kawaida kupatikana kwenye tatuzi nyingi za seva. Tarakilishi viunzikuu za kisasa zikitambulisha IBM zSeries, seva za System z9 na System z10, zinatoa viwango viwili vya kweli isiyo bayana; migawanyo mantiki (LIPARs, kupitia nyenzo PR/SM) na mitambo isiyo bayana (kupitia mfumo tendaji Z/VM).
Wateja wengi wa Viunzikuu wanatumia mashine mbili, moja katika vituo data vyao vya msingi, na moja katika vituo data vya kutunzia nakili za kumbukumbu – kwa utendaji mzima, utendaji kiasi, au inayosubiria – kama ikitokea balaa itakayoathiri mjengo wa kwanza, jaribio, maendeleo, mafunzo, na kazi za uzalishaji wa vitumika na kanzidata zinazoweza kutumika kwenye mashine moja, isipokuwa kwa mahitaji makubwa sana ambapo uwezo wa mashine moja unaweza ukawa na mpaka.

**c)Mini computer**

ni kopyuta ambazo ni ndogo kiumbo zenye bei rahisi,zenye nguvu za wastani kulinganisha na maini fremu,hutumika kwenye taasisi za tafiti na maabara za sayansi.
Aina hizi za kompyuta zilidhihiri katika kipindi cha miaka ya 1960. Ni kompyuta zenye umbile dogo kuliko zile zilizotangulia kutajwa, na ni bora kwa kuunganishia kompyuta nyingine zinazotumika viwandani na ndani ya nchi.

Nazo ni kompyuta za kubeba mkononi, ambazo zimegawanyika katika aina zifuatazo:

- 1. Laptop.
- 2. Notebook.
- 3. Palmtop.

**d)maikro kompyuta**

ni kopyuta ndogo kiumbo yenye bei rahisi isiyo na nguvu sana,hutumika katika tasisi yaku jifunzia kama shule na vyuo. Kompyuta za Kibinafsi (PCs) ambazo ni maalumu kwa ajili ya matumizi ya mtu mmoja tu.Aina hii ya kompyuta inakusanya aina zifuatazo: **Home Computers**, **Portable Computers**

**Aina za maikro kompyuta**

**i)destopu kompyuta**
ni aina ya maikro kompyuta ambayo huwezi kubeba na kutembea nayo imebuniwa kwa ajili ya kukaa mezani

**ii)laptopu kompyuta**
ni aina ya maikro kompyuta inayobebeka na iliyobuniwa kutumika juu ya mapaja

**iii)palm topu kompyuta**
ni aina ya maikro kompyuta ambayo ni ndogo kiasi cha kutosha kwenye mfuko na unaweza kuibeba kiganjani

iv)**Raspberrypi ambao ni mtambo mdogo wa Kompyuta**

## KAZI ZA KOMPYUTA

Kazi za msingi zinazofanyika ndani ya kompyuta ni:

1. Kazi za uingizaji (Input).
2. Kazi za uendeshaji au ufanyishaji (Processing).
3. Kazi za utoaji (Output).
4. Kazi za uhifadhi (Storage

## MGAWANYO YA KOMPYUTA KULINGANA NA DHUMUNI(PURPOSE)

Matumizi ya kompyuta yamegawanyika kulingana na mgawanyo wa mtumiaji mwenyewe
Matumizi ya kompyuta yamegawanyika katika makundi mawili;
i)Matumizi ya jumla
ii)Matumizi maalum

**i) Matumizi ya jumla**;Ni kompyuta zilizoandaliwa kwa ajili ya matumizi yoyote ambayo mtumiaji anaweza kutumia kulingana na matumizi binafsi, mfano mhasibu, mwanasayansi,fundi,mwalimu pia wanafunzi wanaweza kutumia kwa matumizi yao binafsi na kujifunzia.

**ii)Matumizi maalum**;ni matumizi ya kompyuta ambazo hizi zimeundwa kwa malengo maalumu tu kama zile kompyuta zinazoandaliwa kwa ajili ya kuchorea moyo na kupigia x-ray ambazo ni vigumu kwa mtu mwingine kuzitumia kwa kazi zake binafsi.

**MGAWANYO YA KOMPYUTA KULINGANA NA MATUMIZI(FUNCTIONALITY)**

Kompyuta imegawanyika katika makundi matatu kulingana na matumizi,kama ifuatavyo:

a) **Analojia(analogy)kompyuta**

Ni aina ya kompyuta inayotawala taarifa za kianalojia(taarifa zinazoendelea na zisiweza kuhesabika)(non countable and continuous data). Hutumika pia kukotolea arthmetriki operationi(hesabu). Hutumika kutawala analojia data(0 na 1)on and off

Hutumika pia katika ulinganisho wa kilogiki kwa kupima mabadiliko ya mirindimo ya kiumbo.

Mfano hutumika, kupima kasi ya upepo, joto na unyevunyevu.maeneo ambayo hutumia analojia kompyuta ni mamlaka ya viwanja vya ndege na mamlaka ya hali ya hewa.

b) **Dijitali(digital kompyuta**

Ni aina ya kompyuta kulingana na matumizi(function), hutumika kutawala binary number(0 au 1).ni kompyuta zinazotumika kwenye biashara, elimu na sekta za kijamii.

c) **Mahuluti(hybrid)kompyuta**

Ni aina ya kompyuta iliyotengenezwa kwa sifa za analojia na dijitali kompyuta. Hutumia viashiria(signal) vya analojia ili kuzalisha taarifa za kidijitali.

## MAENEO AMBAYO KOMPYUTA HUTUMIKA

***Elimu***

Kutokana na kuendelea kwa elimu ya teknolojia imetusaidia sana kujifunza mambo mbalimbali kupitia kompyuta, ambapo unaweza kuitumia kwa ajili ya kuuliza maswali na kujibiwa kwa haraka tena kwa njia tofauti, kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kielimu, pia unaweza kuandaa vipindi mbalimbali vya masomo na kufundishia elimu tofauti. Pia unaweza kuonyeshea filamu zenye mafundisho mazuri, kama kuonyesha filamu zenye elimu ya jiografia na sayansi ya mifugo na kilimo, kuonyesha sehemu muhimu za nchi, kuonyesha athari za nchi ambazo ndiyo sehemu kuu zinazoleta fedha za kigeni katika nchi, na kuonyesha picha za maendeleo katika sekta mbali mbali za nchi yetu, pia kuonyeshea mila na tamaduni za taifa na mataifa mengine mbalimbali duniani na kadhalika.Kompyuta pia hutumika kusomea vitabu mbalimbali kwa kutumia mtandao.

***Michezo***

Kompyuta zimeandaliwa ndani yake programu mbalimbali zenye michezo tofauti, ambayo inaweza kutumika na watu kulingana na umri wao, na ambayo inajulikana kama moja ya kazi za kukuza kipaji na kuchangamsha akili, na ni sehemu mojawapo ya kuburudisha nafsi.

***Ufundi***

Kompyuta zinaweza kutumika kwa ajili ya kufanyia kazi za ufundi, kama kuchora ramani ya nyumba na mazingira ya nje ya nyumba, kutengenezea picha kwa kuibadilisha na kuiremba na kuifanya ionekane katika sura nyengine ambayo ni tofauti na ile ya asili.

***Mawasiliano***

Kompyuta inaweza kutumika kwa ajili ya kufanyia mawasiliano kupitia mtandao wa (Internet) ambao leo hii ndiyo umeshika nafasi kubwa sana ya mawasiliano kuliko kitu chengine ulimwenguni, kama kuwasiliana kwa kutumiana ujumbe wa barua pepe (E-mail) ambayo ni rahisi na inafika haraka kuliko barua za kupitia posta, pia kwa kutumia barua pepe hakuna haja ya kufikiria sehemu aliko mtu America au bara hindi au sehemu nyingine duniani, kuwasiliana kwa maneno ya maandishi (chat), pia kuwasiliana kwa maneno ya sauti na kuonekana picha (video chat).

***Usafirishaji***

Kwa kutumia kompyuta unaweza kuendeshea kazi za usafirishaji katika vituo vikuu vya usafirishaji, kama usafiri wa ardhini (mabasi, metro na treni), usafiri wa majini (meli), na usafiri wa angani (ndege).

***Matumizi ya kiwandani***

Kama kuendeshea mashine viwandani kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbali mbali, kama kutengenezea magari, kuzalishia umeme na kutengenezea bidhaa nyengine za kawaida kama nguo mazulia na kadhalika.Kompyuta hizi zina utofauti kidogo na zile nyingine hasa kwa sababu huwazimebuniwa na kuundwa kufanya operesheni fulani kulingana na kiwanda na zina uwezo wa kufanya kazi kwa mazingira magumu kuliko kompyuta ya kawaida kama vile mazingira yenye joto, vumbi, kemikali, mvuke, au baridizaidi.

***Matumizi ya benki***

Kama ilivyokuwa ada na kawaida hivi sasa kutumia kompyuta kwa ajili ya kuendeshea kazi za benki,kwa ajili kurahisisha kazi za mahesabu.

***Matibabu***

Kompyuta zimekuwa na matumizi makubwa na muhimu sana katika kufanyia uchunguzi na matibabu hospitalini, kama kuchunguza na kuelekeza dawa ya kutibu ugonjwa uliyoonekana, pia kupimia na kujaribia mimba na kutoa maelekezo kuhusiana na siku na tarehe ya kujifungua.

**USALMA NDANI YA KARAKANA YA COMPYUTA**

**A. Tabia za kuzingatia unapokuwa ndani ya karakana ya compyuta**

i. Epuka uvutaji wa sigara,marjuana au moshi wa namna yoyote ile kwa sababu moshi au vumbi huathiri/kuharibu kompyuta

ii. Epuka kubeba vyakula na vinywaji wakati unaingia katika maabara ya kompyuta

iii. Epuka mijongeo isiyo kuwa ya kawaida

iv. Fuata njia sahihi za kuwasha na kuzima kompyuta

v. Ajali zinazotokea ndani ya maabara ya kompyuta inapaswa kufikishwa kwa mhusika wa maabara kwa haraka zaidi

vi. Kama huna uhakika wa ubebaji wa vifaa vya kompyuta unapokuwa maabara omba msaada kutoka kwa muhusika

**B. uingiaji na utokaji wa hewa katika maabara ya compyuta**

maabara ya kompyuta ni muhimu iwe na vipitisha hewa ambavyo vitawezesha muzunguko wa hewa kuwa tulivu kwa ajili ya vifaa vya kompyuta(air motion)

**C. mwanga ndani ya maabara ya kompyuta**

maabara ya kompyuta inapaswa kuruhusu mwanga wa kutosha ili kuondoa matatizo ya macho kwa mtumiaji ambayo yanaweza kumpelekea maumivu ya kichwa msongo na uchovu. Mtumiaji wa kompyuta anatakiwa kupunguza mwanga kwenye muwazi mpaka pale macho yatakapo ona vizuri

**D. Usalama dhidi ya moto unapokuwa kwenye mabara ya kompyuta**

maabara ya kompyuta inatakiwa iwe na vikinga moto(fire extinguisher)kusaidia kuokoa vifaa

E. **Usalama dhidi ya vumbi na maji**

Maabara ya kompyuta inatakiwa kuwa na mapazia ambayo yatazuia uingiaji wa vumbi na matone ya maji

F. **Samani kwenye maabara ya kompyuta**

meza na viti vinapaswa kuwa imara ili visisababishe udondokaji wa vifaa vya kompyuta

G. **Usalama katika uingiaji kwenye maabara ya kompyuta**

a) Weka kufuri,mlango na madirisha imara ili kulinda vifaa vilivyomo ndani

b) Usikaribishe mgeni usiye mfahamu au asiye muhusika wa maabara/chumba cha kompyuta

c) Weka (alam securty)king'ora cha usalama kwa ajili ya hatari itokeapo

H. **Umeme(stable power)**

Maabara ya compyuta inahitaji umeme toshelevu kwa ajili ya vifaa

**MGAWANYO WA MFUMO WA KOMPYUTA**

Kompyuta imegawanyika katika sehemu kuu mbili

1. Sehemu zinazoshikika(hardware)

2. Sehemu zisizoshikika(soft ware)

**1. SEHEMU ZINAZOSHIKIKA(HARDWARE)**

Ni sehemu zinawezakushikwa na kuonenakana kwa macho mfano keyboard ,mouse,kicharazio.

***i)vifaa vinavyoingiza taarifa ndani ya kompyuta (input device)***

a) kibao bonye/baobonye
b) puku/kipanya
c) skana
d) microphone
e) camera

**keyboard/Bao bonye**

hutumika kuingiza namba, herufi na alama za uandishi ndani ya kompyuta,ni kifaa kinachotumika kuingiza data(input data) kwenye mfumo wa kompyuta.

keybord imegawanyika katika sehemu kuu nne:

a) Funguo za kuandikia(type writer keys)
b) Funguo za kuhama(movement keys)
c) Funguo za namba(numericaly keys)
d) Funguo za kazi(function keys)




***Jina la funguo Kazi yake***

☆ Kibonyezo (cha) nyumbani ‘home key' Inatumika kwa ajili ya kuhamia mwanzo wa mstari ☆End Inatumika kwa ajili ya kuhamia mwisho wa mstari.

☆ Inatumika kwa ajili ya kuhamia juu ya mstari

☆ Inatumika kwa ajili ya kuhamia upande wa kushoto mwa mstari

☆ Inatumika kwa ajili ya kuhamia upande wa kulia mwa mstari.

☆ Inatumika kwa ajili ya kuhamia chini ya mstari.

☆ kibonyezo (cha) ukurasa uliotangulia Inatumika kwa ajili ya kuhamia juu ya mstari.

☆ Kibonyezo (cha) ukurasa unaofuata Inatumika kwa ajili ya kuhamia chini ya mstari.

☆ Kibonyezo (cha) mahesabu ‘numeral key’ Inatumika kwa ajili ya kufunga na kufungulia namba na michoro.

☆ Kibonyezo (cha) herufi kubwa ‘caps lock’ Inatumika kwa ajili ya kufunga na kufungulia.

☆ Kibonyezo (cha) kuendelea ‘enter key’ Inatumika kwa ajili ya kutekeleza amri, au kuanzisha fungu la maneno kwenye ukurasa..

☆ Kibonyezo (cha) kufutia ‘delete key’ Inatumika Kwa ajili ya kufuta herufi ya mbele yake.

☆ Kibonyezo (cha) kirejeshi ‘back space’ Inatumika Kwa ajili ya kufuta herufi ya nyuma yake.

☆ Kibonyezo (cha) nafasi ‘space bar’ Inatumika Kwa ajili ya kuweka masafa kati ya maneno.

☆ Kibonyezo (cha) kiepushi ‘escape key’ Inatumika kwa ajili ya kuacha kutekeleza amri.

☆ Kibonyezo (cha) mpangilio ‘tab key’ Inatumika kwa ajili ya kuwacha masafa maalumu tofauti na ya kawaida (Normal).

☆ Kibonyezo (cha) kudhibiti ‘control key’ inatumika daima pamoja na ufunguo mwengine kwa ajili ya kutekeleza amri maalumu.

☆ Kibonyezo (cha) kibadalishi ‘alt(ernate) key’ inatumika daima pamoja na ufunguo mwengine kwa ajili ya kutekeleza amri maalumu.

☆ Kibonyezo (cha) kuhama ‘shift key’ inatumika daima pamoja na ufunguo mwengine kwa ajili ya kutekeleza amri maalumu.

☆ Alt-Shift Inatumika kwa ajili ya kubadilishia lugha.

☆ Ctrl-Shift Inatumika kwa ajili ya kubadilishia mwelekeo ndani ya ukurasa (kulia au kushoto)

☆ Print screen Inatumika kwa ajili ya kupiga picha kitu chochote kwenye kompyuta.

☆ Ctrl-Alt-Del Inatumika kwa ajili ya kuwasha upya kompyuta.

**Kipanya(mouse)**

Kitufe cha kushoto hutumika kuchagulia maandishi /maneno hutumika kuchagulia orodha.Kuna vitufe viwili kwenye kila mausi, kitufe cha upande wa kushoto (Left click) kinatumika kufungulia windozi, programu na kuchagulia maandishi, maneno na picha, na kitufe cha upande wa kulia (Right click) kinatumika kufungulia orodha ya mapendekezo ya kazi.

**MBINU ZA KUTUMIA KIPANYA/KISAKURA(MOUSE TECHNIQUES)**

- ◊ **BOFYA(CLICKING)**

Ni ubofyaji na uachiaji wa kitufe cha kushoto mara moja

- ◊ **BOFYA MARA MBILI(DOUBLE CLICKING)**

Ni kitendo cha ubofyaji wa kitufe cha kushoto mara mbili

- ◊ **BOFYA KITUFE CHA KULIA(RIGHT CLICKING)**

Ni ubofyaji wa kitufe cha kulia mara moja

- ◊ **UBURUZAJI NA UACHIAJI(DRAG AND DROP)**

Ni kitendo cha kuiburuza mouse huku umebana kitufe cha kushoto,kisha kuiachia hutumika kuamisha faili,picha au folda kutoka eneo moja kwenda eneo jingine.

**Scana**

Hutumika kuingizia nyaraka ngumu (hard copy)ndani ya kompyuta. Skana inatumika kwa ajili ya kuingizia picha ndani ya kompyuta. Na kitu chochote kile kinachoingia ndani ya kompyuta kwa njia ya skana kinapewa sifa ya picha.

**Microphone**

Hutumika kuingiza sauti ndani ya kompyuta, Makrofoni inatumika kwa ajili ya kuingizia sauti ndani ya kompyuta.

**Camera**
Hutumika kupiga picha na kuingiza ndani ya kompyuta

***ii) Vifaa vya kutolea vitu(output device)***
ni vifaa vya pembeni(peripherial device) ambavyo kompyuta hutumia ili kutolea habari baada ya uchakataji.

**AINA ZA VIFAA VYA KUTOLEA HABARI**

- **Soft copy(kopi laini)**

Ni matokeo ya taarifa zilizochakatwa ambayo hayashikiki na huonyeshwa kwenye skrini na kupitia kwenye spika kama sauti.

- **Hard copy(kopi ngumu)**

Ni matokeo ya taarifa zilizochakatwa ambayo yanashikika na huzalishwa kwenye karatasi kwa kutumia printers ama plotta.

**Skrini(monitor)**
Inatumika kuonyesha matokeo yavitu vinavyofanyika ndani ya kompyuta

**Monitor/muwazi**

**AINA ZA MUWAZI/MONITOR**

**MGAWANYO KULINGANA NA RANGI INAYESHWA (ACCORDING TO DISPLAY)**

**1**, **Monochrome monitor**
Hutumika kuonyesha neno /maneno na picha kwa rangi moja tu na kijani na bluu.

**2, colour monitor**
Huonyesha neno /maneno na picha kwakutumia rangi tofauti tofauti .

**Aina za muonekano wa skriin ya kiwambi**

**a) Cathode ray tube**

Ni kiwambi chenye skriini inayoonekana katika umbo la curve, hutumia kiasi kikubwa cha umeme na si rahisi kubebeka.

**b) Flat panel screen**

Ni kiwambi chenye skriini inayoonekana katika umbo la flat, hutumia kias kidogo cha umeme,huonyesha picha angavu. Mfano LCD,TFT ,EL na gas plasma

**Kipaza sauti-**hutumika kutolea sauti ndani ya kompyuta

**Printer-**hutumika kutolea vitu vya maandishi au picha kwenye kompyuta.

**Kipaza sauti (speaker)**

Kipaza sauti kinatumika kwa ajili ya kutolea sauti kutoka ndani ya kompyuta.

**Printa (printer)**

Printa inatumika kwa ajili ya kutolea vitu vya maandishi au picha kwenye kompyuta kwa njia ya karatasi (kuchapisha).

**Plota (ploter)**

Plota ni chombo kinachotumika kwa ajili ya kutolea vitu, ambacho kinafanana na printa katika ufanisi wake wa kazi, lakini umbile lake ni kubwa kuliko printa, na kinatumika kwa ajili ya kuchapishia picha na michoro ya kiufundi, pia kinaweza kutumika kwa ajili ya kuchapisha maandishi kama herufi namba na alama.

**Kadi ya sauti**
Kadi ya sauti ni sehemu ya tarakilishi inayotoa sauti katika kipazasauti cha tarakilishi.

**Kadi ya mtandao**
Kadi ya mtandao ni sehemu ya tarakilishi inayoruhusu kutumia intaneti.

**Kadi mchoro**
Kadi mchoro ni sehemu ya tarakilishi inayotoa picha katika kiwambi cha tarakilishi.

**SEHEMU ZISIZOSHIKIKA (SOFTWARE)**
Kompyuta haiwezi kufanya kazi mpaka kipatikane kitu kinachoitwa software, ambacho kinawakilisha programu zinazoendesha kompyuta. Programu hizo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili:

- ✓ **Programu za kuendeshea kompyuta (operating systems)**

programu hizo zinaitwa Windows, na kuna aina nyingi za Windows kulingana na toleo lake na ubora wake, kwani siku zinavyozidi kwenda mbele ndipo tunapozidi kupokea programu nyingine za Windows zenye ubora zaidi kuliko zile za awali.

**KAZI ZA SISTIMU SOFTIWEA (SYSTEM SOFTWARE) AU OPARETING SYSTEM**

- ➢ Kuongoza shughuli zote za kompyuta
- ➢ kuonesha makosa ya kiundishi
- ➢ kuunganisha softiwea (softiwer)na hadiwea(hardware)
- ➢ kusaidia katika uzimaji na uwashaji wa kompyuta
- ➢ kusaidia mawasiliano baina ya aplikesheni na aplikesheni( application moja na nyingine)

- ✓ **Programu za kufanyia kazi (Application systems)**

nazo ni: Microsoft Office na Graphics design; programu hizo daima zinafanya kazi ndani ya windows, ambazo zinatumika kwa ajili ya kazi mbalimbali za uandishi na hesabu, na kazi nyinginezo za kuunda na kutengeneza picha n.k.
***Vifaa vya kuendeshea vifaa vya kuingizia na kutolea vitu***:

Vifaa hivi vipo ndani ya chombo kiitwacho C.P.U. (kifupi cha Central Processing Unit), ambacho ni kiini cha kompyuta na ndicho kinachofanya kazi ya kuviendesha vifaa vyote vya kompyuta na kutoa maelekezo yote. C.P.U. ni sehemu kuu ya nguvu ya kompyuta, au kitovu cha kompyuta. Kazi za C.P.U. ni:

***Kutawala (Control)***

Ndani ya madhabodi (Motherboard) kinapatikana kifaa kinachoitwa Bios (kifupi cha Basic Input Output System), ambacho ndicho kinachofanya kazi ya kuviendesha vifaa vya kuingizia na kutolea vitu. Ni vigumu kufuta au kurekebisha vitu vilivyomo ndani ya kifaa hicho kwani vinazingatiwa ni vitu vya kusomea tu na si kwa kazi nyingine.Kazi za mahesabu ni kazi zote zinazofanywa na hesabu, kama vile kutoa, kujumlisha, kuzidisha na kugawanya.

***Sytem unit ni mfumo mkuu/nyumba ya mfumo wa kompyuta inayoundwa na vitu vifuatavyo;***

- ✓ **Power supply**

Hutumika kuruhusu umeme kuingia kwenye mfumo wa kompyuta kwa ujumla na vifaa vya kupokelea taarifa kama kiwambi/monitor.

- ✓ **System board/circuit board/motherboard**

Ni sakiti kuu iliyoshikizavifaa vya kompyuta ndogo,hujumuisha microprocessor chips,main memory chips,expansion slots ambayo uunganisha na huchomeka vifaa vingine.

- ✓ **Storage device(vifaa vya kuhifadhia)**

Hujumuisha floppy disk(diskette), CD,mfumo wa muziki, disk ngumu

## VIFAA VYA KUHIFADHIA TAARIFA NA HABARI (STORAGE DEVICE)

Ni vifaa vinavyotumika kuhifadhi taarifa na habari zinazotumwa kwenye mfumo wa kompyuta
Aina za uhifadhi(storage)

- ❖ **PRIMARY STORAGE**

Ni aina ya uhifadhi inayotumika kuhifadhi taarifa kwa muda mfupi(short time) kabla ya kuhifadhiwa kwenye secondary storage.mfano wa taarifa zinazohifadhiwa kwenye memory.
Aina za memory

- o **Read only memory(ROM)**

Ni memory inayotumika kuhifadhi programu na maelekezo yake pamoja na taarifa permanently(moja kwa moja). Taarifa zinazohifadhiwa kwenye memory hii hua zinakaa kwa muda mrefu bila kubadilishwa.
Aina za read only memory

- ◊ **MROM(Mask Read Only Memory)**

Ni taarifa zinazohifadhiwa na kuandikwa na mtunzaji,mtengenezaji haziwezi kubadilishwa.

- ◊ **Programmable read only memoery(PROM)**

Memory hii humruhusu mtumiaji kuhapia mara tu baada ya kuandikwa ndani mwake.

- ◊ **Erasable programmable read only memory(EPROM)**

Taarifa zinazohifadhiwa kwenye memory hii zinaweza kufutwa mara zinapokutana na mionzi ya ultra violent na hupangiliwa upya kwa matumizi mengine.

- ◊ **Electrically erasable programmable read only memory(EAPROM)**

Ni memory ambayo unaweza kufuta na ukapanglia kwa kutumia umeme.

- ❖ **SECONDARY STORAGE**

Ni aina ya uhifadhi inayotumika kuhifadhi taarifa ambazo zimehidhinishwa na primary storage. Hutumika kuhifadhi taarifa kwa muda mrefu. Hutambulika kama memory kuu.

## UPIMAJI UKUBWA WA VIFAA UTUNZAJI TAARIFA (MEASUREMENT OF STORAGE DIVICES)

Kumbukumbu ya kompyuta hupimwa kwa Byte,kilobyte,megabyte,gigabyte,au terabyte byte ni kiasi cha nafasi unayohitaji kuhifadhi herufi  kuanzia moja kiasi kizuri kinacho hitajika ni Petra byte ambacho huwa na uwezo wa kuhifadhi mamilioni ya herufi

## VIPIMO MBALIMBALI VYA UKUBWA

1024 Bytes= 1 kilobyte (KB)

1024 kilobyte (kb) =1 megabyte (MB)

1024 megabyte (mb)=1gigabyte (GB)

1024 gigabyte (gb) =1terabyte (TB)

1024 Terabyte (tb)= 1petabyte (PB

**Kuanza kutumia Windows**

Kabla hujaanza kutumia Windows unatakiwa kufanya mambo yafuatayo:

1. Kuhakikisha waya wa umeme umeshaunganishwa kwenye kompyuta yako.
2. Kufungua kompyuta kwa kutumia sehemu inayoitwa power.
3. Kusubiri mpaka idhihiri sehemu inayoitwa desktop.

**BOOTING**

Ni mchakato ambao kompyuta husukuma(loads) mafile kuyapeleka katika memory kuu ya kompyuta

**AINA ZA BOOTING**

- **COLD BOOTING**

Ni mchakato wa kuwasha kompyuta iliyozimwa moja kwa moja kwa kubonyeza kitufe cha kuwashia.

- **WARM BOOTING**

Ni mchakato unahohusisha kuzima na kuwasha(restart) kwa kompyuta iliyowaka,hutumia kitufe cha kuwashia na kuzimia(restart button).

**Bei ya tarakilishi**

Hakuna bei haswa ya tarakilishi. Bei huenda ikawa juu au chini kulingana na aina (model), uwezo wa kuhifadhi data, ukubwa wa diski, ukubwa wa RAM, spidi ya procesa na programu ambayo kompyuta yaweza kuzitumia.

**FAIDA ZA MATUMIZI YA KOMPYUTA KATIKA SHUGHULI MBALIMBALI**

- Inatatua tatizo lolote kulingana na maelekezo inayopewa
- Inauwezo wa kurudisha taarifa ambazo zimepotea kwa kiasi kikubwa.
- Inauwezo wa kuwasiliana na mifumo mingine kupitia mtandao

- Kujiajili/utengenezaji wa  ajira kwa watu wanaotumia na kufahamu
- Kompyuta huwezesha mawasiliano baina ya mtu eneo moja na eneo jingine.
- Hurahisisha mawasiliano
- Kompyuta inafanya kazi kwa muda mrefu bila kuchoka
- kompyuta inafanya kazi kwa muda na spidi ya hali ya juu ukilinganisha na binadamu
- kompyuta inauwezo mkubwa wa kuhifadhi taarifa.
- kompyuta inauwezo wa kusafirisha taarifa kwa haraka zaidi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine
- kompyuta inauwezo mkubwa wa kufungua taarifa kwa haraka.

**HASARA ZA MTUMIAJI WA KOMPYUTA (DISADVANTAGE OF COMPYUTER)**

- kompyuta ni ghali (costful) katika matengenezo
- kompyuta inaweza kusababisha matatizo ya macho
- kompyuta inaweza kusababisha uhalibifu wa misuli ya kichwa kwasababu ya utumiaji wa muda mrefu
- kompyuta huathiriwa na vumbi, joto na maji
- utumiaji wa programu isivyotakiwa hupelekea uvunjifu wa maadili(utumiaji wa mtandao wa intaneti)

